JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

## 612 URAIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

# 612 URAIA

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Dola ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Upimaji na Tathmini ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu ........ 6
2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia ........ 8
2.1.5 Swali la 5: Dola ........ 10
2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia ........ 12
2.1.7 Swali la 7: Zana za kufundishia na kujifunzia ........ 15
2.1.8 Swali la 8: Uchumi wa Tanzania ........ 16
2.1.9 Swali la 9: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia ........ 19
2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya Kufundisha somo la Uraia ........ 21
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ........ 24
2.2.1 Swali la 11: Dola ........ 24
2.2.2 Swali la 12: Utamaduni Wetu ........ 29
2.2.3 Swali la 13: Uhusiano wa Kimataifa ........ 33
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu) ........ 36
2.3.1 Swali la 14: Uchambuzi wa Mchapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia ........ 37
2.3.2 Swali la 15: Zana za kufundishia na Kujifunzia ........ 40
2.3.3 Swali la 16: Upimaji na Tathmini ........ 44
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........ 48
4.0 HITIMISHO ........ 48
5.0 MAPENDEKEZO ........ 49
*Kiambatisho* ........ 50

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la III mwaka A mwaka 2020 kwa somo la Uraia. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanachuo, wakufunzi, waandaaji sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Watahini wa somo na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Uraia kwa Watahiniwa wa Ualimu ngazi ya Astashahada ulifanyika mwezi Julai, 2020 na uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa mwaka 2009.

Mtihani ulikuwa na maswali kumi na sita (16) na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14) kutoka katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B na C zilikuwa na maswali matatu (03) kila moja ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili kutoka kila sehemu. Kila swali katika sehemu B na C lilikuwa na alama 15.

Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Uraia kwa mwaka 2020 ulikuwa mzuri ambapo asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 40 na zaidi. Kati yao, asilimia 55.14 walipata daraja A, asilimia 40.73 daraja B, asilimia 3.95 daraja C, asilimia 0.14 daraja D na mtahiniwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.02 daraja F. Ufaulu huu umepungua kwa asilimia 0.01 ikilinganishwa na mwaka 2019, ambapo asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mthani walipata wastani wa alama 40 na zaidi. Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni 'vizuri', 'wastani', na 'hafifu'. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa Uraia. Sampuli za majibu yao zimeambatishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa inaonesha pia sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kwa mada hizo ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 3 hadi 4.

#### 2.1.1 Swali la 1: Dola


Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kifupi kuchambua aina nne za wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya watahiniwa 5,430 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 105 (1.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 204 (3.8%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 5,121 (94.3%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Watahiniwa (94.3%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Dola hususan kipengele cha Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Watahiniwa hao walielewa vema matakwa ya

swali na hivyo kutoa majibu sahihi. Mfano wa majibu hayo ni; *Wabunge waliochaguliwa kutoka kwenye majimbo, Wabunge wa kuteuliwa na Rais, Wabunge wa viti maalumu (wanawake), Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar* na *Mwanasheria Mkuu*. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



1. Aina za wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni

(a) Wabunge wa kuchaguliwa
Ni wabunge wanaochaguliwa na wananchi kutoka kwenye majimbo ya Uchaguzi.

(b) Wabunge wa kuteuliwa
Ni wabunge ambao huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


(c) Wabunge wa viti maalum
Ni wabunge ambao huchaguliwa na wanawake ili kutatua na kuwakilisha kero zao.

(d) Wabunge kutoka Baraza na Uwakilishi zanzibar: Hushughulikia masuala ya kimapinduzi.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Aidha, watahiniwa (3.8%) waliopata ufaulu wa wastani walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao. Wengi walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa majibu pungufu au maelezo dhaifu na hivyo kushindwa kupata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja mbali na kutoa majibu mawili sahihi alitaja pia majibu yasiyo sahihi kama; *wabunge wa kurithi* na *wabunge wa kuombwa* hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 1.9 ya watahiniwa waliopata alama hafifu katika swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika hivyo, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine (0.6%) waliopata alama 0 walionesha kutokuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi kama; *Spika wa Bunge, Naibu Mbunge* na *Naibu Waziri Spika*. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.



(1) kwa kifupi chambua aina nne za wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(i) Jaji Mkuu
(ii) Spika wa Bunge
(iii) Mbunge wa wilaya.
(iv) Mbunge wa alimashauri kuu.

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa alitaja viongozi wa Mahakama na Bunge pamoja na kutaja vyeo vya wabunge visivyo sahihi badala ya kuchambua kwa kifupi aina za wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


### 2.1.2 Swali la 2: Upimaji na Tathmini

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi aina nne za tathmini katika ufundishaji. Swali hili lilifanywa na watahiniwa wote 5,430 sawa na asilimia 100. Kati yao, watahiniwa 85 (1.6%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 419 (7.7%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 5,025 (90.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 98.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*


Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kueleza kwa kifupi aina tatu hadi nne za tathmini katika ufundishaji. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana nzima ya *Upimaji na Tathmini* na hivyo kutoa majibu sahihi kama*; tathmini awali - hii ni tathmini inayopima uwezo wa mwanafunzi kumudu kuanza masomo mapya*, *tathmini dodoso/tatuzi hii hutafuta chanzo cha tatizo*, *tathmini endelevu hii hufanyika wakati wote katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo* na *tathmini tamati hufanyika mwishoni mwa kozi au mafunzo*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


2. i) Tathmini awali ni aina ya tathmini ambayo hufanyika mwanzoni mwa mafunzo Kubaini maarifa ya awali aliyonayo mwanafunzi.
ii) Tathmini endelevu ni aina ya tathmini ambayo hufanyika wakati wote wa mafunzo.
iii) Tathmini tatuzi ni aina ya tathmini ambayo hutumika Kubaini chanzo cha tatizo katika ujifunzaji na namna ya Kukabiliana na tatizo hilo.
iv) Tathmini tamati ni aina ya tathmini ambayo hufanyika mwishoni mwa mafunzo. mfano darasa la 7.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2

Aidha, kwa watahiniwa (7.7%) waliokuwa na ufaulu wa wastani, kati yao wapo waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine waliweza kutaja aina zote za tathmini bila kutoa maelezo kwa ufupi na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5 kati yao watahiniwa wachache (0.8%) waliweza kutaja aina moja ya tathmini na wengine kutaja aina mbili hadi tatu za tathmini bila maelezo. Aidha, watahiniwa (0.8%) ambao walipata alama 0, kati yao walikuwepo ambao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusiana na dhana ya *Upimaji na Tathmini*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama: *tathmini ya mwanafunzi, tathmni ya mwalimu, tathmni ya Mwalimu Mkuu na tathmini ya Mkuu wa Idara*, majibu ambayo si sahihi kwa mujibu wa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.



2. i) Tathimini ya mwalimu
ii) Tathimini ya mwanafunzi
iii) Tathimini ya upimaji katika elimu.
iv) Tathimini katika mithiani.

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika baadhi ya vipengele vya andalio la somo na kuchanganya na tathmini mbalimbali katika mfumo wa elimu badala ya aina za tathmini katika ufundishaji, na hivyo kupata alama 0

### 2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu


Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne yanayoathiri utendaji kazi katika jamii. Kati ya watahiniwa 5,430 waliofanya swali hili, watahiniwa 51 (0.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1, watahiniwa 25 (0.5%) walipata alama 2 na watahiniwa 5,354 (98.6%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4.


Watahiniwa (98.6%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Utamaduni Wetu,* hususan mada ndogo ya *Kazi*. Watahiniwa hao waliweza kutoa majibu sahihi kwa kutaja majibu matatu hadi manne kama: *rushwa, mmomonyoko wa maadili, urasimu, miundo mbinu mibovu kama usafiri, umeme na maji* na *uzembe/uvivu wa kutojali*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuelewa matakwa ya swali kama inavyoonekana kwenye sampuli ya jibu la mtahiniwa kwenye Kielelezo Na. 3.1.


3. i) Utumiaji wa madawa ya kulevya kwa vijana
ii) Rushwa (kutoa rushwa na kupokea rushwa)
iii) Mmomonyoko wa maadili.
iv) Ulevi.

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3

Aidha, watahiniwa (0.5%) waliopata alama za wastani katika swali hili, walidhihirisha kuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama: uchanganyaji wa majibu sahihi na yasiyo sahihi, utoaji wa mambo pungufu ya manne yaliyohitajika kwenye swali na kurudia majibu. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya wastani katika mada husika hivyo kushindwa kutoa majibu yaliyohitajika kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja pamoja na majibu mawili sahihi, alitoa pia majibu yasiyo sahihi kama: *kutokuwa na huruma* na *kutumia madawa*; bila maelezo yoyote na hivyo kupata alama za wastani.


Kwa upande mwingine watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao walishindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa majibu pungufu na yenye udhaifu. Watahiniwa (0.8%) waliopata alama 0 walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja badala ya kutaja mambo manne yanayoathiri utendaji kazi katika jamii alitoa majibu yanayoonesha sababu za kudumaa kwa maendeleo katika nyanja mbalimbali kwenye jamii kama; *mwingiliano wa madaraka, kutokuwepo kwa umoja na mshikamano, matabaka kati ya viongozi na ufujaji wa mali za umma* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 3.2.




Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

### 2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo manne ya kuzingatia katika ufundishaji wa mada ngumu katika somo la Uraia. Miongoni mwa watahiniwa 5,430 waliofanya swali hili, watahiniwa 1,417 (26.1%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa 1,472 (27.1%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,541 (46.8%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 73.9 walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

Watahiniwa (46.8%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kubainisha mambo matatu hadi manne ya kuzingatia katika ufundishaji wa mada ngumu katika somo la Uraia kama; *kuzingatia matumizi ya zana za kufundishia na*

*kujifunzia, kuzingatia matumizi ya njia shirikishi, kutumia uzoefu walionao wanafunzi pamoja na maarifa/stadi walizonazo wanafunzi* na *kuhakikisha ufundishaji unawiana na utamaduni wa wanafunzi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

04. Mambo ya kuzingatia katika ufundishaji wa mada ngumu katika somo la uraia

i) Uhusiano wa mada na uzoefu wa mwanafunzi
Mwalimu anatakiwa ahusianishe mada na mazingira ya mwanafunzi ili aweze kuelewa mfano mada ya uchumi wetu.

ii) Matumizi ya zana wakati wa kufundisha
Mwalimu anatakiwa atumie zana ambazo zinaendana na mada inayofundishwa ili mwanafunzi aweze kuelewa.

iii) Kutumia mbinu bora katika kufundishia
Mwalimu anatakiwa atumie mbinu bora katika kufundisha mada ngumu. mfano ziara mafunzo.


iv) kumpatia mwanafunzi kazi iliaweze kuchunguza mambo yanayofanyika katika jamii yake
mwalimu kumpatia mwanafunzi kazi ya kujifunza ambayo itamfanya achunguze mambo mambayo yanatendeka katika jamii mfano kuchunguza aina za familia, mila na desturi za jamii yake.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4

Aidha, watahiniwa (27.1%) waliopata alama za wastani walielewa matakwa ya swali isipokuwa walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu dhana nzima ya *ufundishaji wa mada ngumu katika somo la Uraia* na hivyo kushindwa kutoa majibu yote manne kwa usahihi na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (26.1%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo

kutoa majibu dhaifu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa wengine waliopata alama 0 walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana husika na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *upangaji mzuri wa darasa, darasa kuwa tulivu, kuwauliza wanafunzi kama wameelewa* na *matumizi ya lugha nzuri darasani*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekwenda kinyume na matakwa ya swali.




4. (a) Uzingatiaji wa malengo mahususi
(b) Uzingatiaji wa umri wa mwanafunzi
(c) Uzingatiaji wa uelewa na idadi ya wanafunzi
(d) Uzingatiaji wa ukubwa wa darasa.

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa aliandika mambo ya kuzingatia katika utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia badala ya mambo ya kuzingatia katika ufundishaji wa mada ngumu katika somo la Uraia.


### 2.1.5 Swali la 5: Dola

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi faida nne za Serikali za Mitaa katika maendeleo ya jamii. Miongoni mwa watahiniwa 5,430 waliofanya swali hili, watahiniwa 27 (0.5%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 69 (1.2%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 5,337 (98.3%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.5 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5*

Watahiniwa wengi (98.3%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kueleza kwa kifupi faida nne za Serikali za Mitaa katika maendeleo ya jamii kwa kutoa hoja kama; *kuimarisha utawala bora, kukusanya mapato, kushiriki katika shughuli mbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi* na *kutoa huduma za jamii kwa urahisi na ukaribu zaidi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Serikali za Mitaa* na walielewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



5 - Kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa miundombinu katika mitaa. Mfano madarasa majengo ya shule.
- Kukusanya kodi katika mitaa mbalimbali. Mfano kodi ya sehemu ya biashara kwa wananchi
- Kuimarisha ulinzi katika mitaa wakati wa usiku. Mfano uwepo wa Sungusungu.
- Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa maendeleo ya jamii katika ushiriki heri. Mfano kutoa fursa za ujasiriamali.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5

Aidha, asilimia 1.2 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama; kutoa hoja pungufu ya tatu, kuchaganya hoja sahihi na zisizo sahihi na maelezo yasiyojitosheleza katika majibu yote yaliyosababisha wapate kuanzia alama 2 hadi 2.5.

Watahiniwa (0.5%) waliopata alama hafifu katika swali hili, baadhi yao walionesha kutokuelewa matakwa ya swali, hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi yaliyosababisha wapate alama 1 au 1.5. Watahiniwa wengine (0.3%) waliopata alama 0 wengi hawakuwa na maarifa kuhusu dhana nzima ya *Serikali za Mitaa* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


| | |
|---|---|
| 5. | i) Kusikiliza na kuamua kesi Mbalimbali |
| | ii) Kusaini fomu Mbalimbali za Mikopo. |

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.2 mtahiniwa ametoa hoja za kubuni ambazo si kazi za msingi za Serikali za Mitaa bali ni majukumu ambayo yanaweza kufanywa na taasisi za kifedha, polisi au mahakama.


### 2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia

Mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha faida nne za kuoanisha Katiba na mada za somo la Uraia katika ufundishaji na ujifunzaji. Kati ya watahiniwa 5,430 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 695 (12.8%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 630 (11.6%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 4,105 (75.6%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 87.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

Asilimia 75.6 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kuorodhesha faida tatu hadi nne za kuoanisha Katiba na mada za somo la Uraia katika ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na wanafunzi hao ni kama; *husaidia kufundisha Katiba hivyo wanafunzi wataweza kuijua na kuifuata, kujenga mazoea ya kusoma Katiba, husaidia kujua muundo wa dola* na *kutambua haki na wajibu wa raia*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.




06· Faida nne za kuoanisha Katiba na mada za somo la Uraia katika ufundishaji na ujifunzaji.
(i) Husaidia kuwajengea wanafunzi mazoea ya kusoma Katiba mara kwa mara.
(ii) Husaidia wanafunzi kuipitia na kuielewa Katiba ya nchi.
(iii) Husaidia kujua nchi inavyoendeshwa kwa kufuata Katiba na sheria za nchi kwa ujumla.
(iv) Husaidia kujua sheria za nchi kwa kina zaidi.

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6

Aidha, watahiniwa (11.6%) waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 baadhi yao waliandika majibu pungufu ya manne yaliyohitajika kwenye swali na wengine walirudia jibu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja zisizo sahihi kwenye majibu yake kama; *kulinda mipaka ya nchi* na *kuimarisha maslai* ambayo hayakuwa majibu sahihi.

Hata hivyo, watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana nzima ya *Uhusishi wa mada za Uraia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania* na hivyo kuorodhesha hoja 1 au mbili zenye dosari zilizo sababisha kupata alama 1 au 1.5. Watahiniwa (5.1%) waliopata alama 0 hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 6.2.




06 Faida nne(4) za maswali ya kuoanisha
(i) Hupima Sehemu kubwa ya maudhui
(ii) Ni rahisi katika usahihishaji
(iii) Hupima ufahamu wa mwanafunzi
(iv) Maswali ya namna hii ni rahisi kuyatunga

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali 6

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa aliorodhesha faida za maswali ya kuoanisha badala ya faida za kuoanisha Katiba na mada za somo la Uraia katika ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kupata alama 0.


### 2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Mtahiniwa alitakiwa kutaja mbinu nne za kupata zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia. Miongoni mwa watahiniwa 5,430 waliofanya mtihani, watahiniwa 276 (5.1%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 457 (8.4%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 4,717 (86.5%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 94.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*


Asilimia 86.5 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kutaja mbinu tatu hadi nne za kupata zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Upatikanaji wa zana*, hivyo waliweza kupata alama nzuri katika swali hili. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa ni kama; *kununua, kutengeneza, kuazima, kufaragua* na *kukodi toka kwenye taasisi mbalimbali*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


7. i) Kutengeneza
ii) Kufaragua
iii) Kuazima
iv) Kununua.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walionesha mapungufu katika majibu yao. Baadhi yao walitaja mbinu pungufu ya tatu na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (5.1%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao walitaja mbinu pungufu ya mbili na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo kupata alama 1 au 1.5. Katika kundi hili, walikuwepo waliorudia majibu, kwa mfano mtahiniwa mmoja alitaja; *kushona*, *kusuka*, *kutengeneza* na *kufinyanga* bila kujua kuwa majibu yote hayo yanaingia kwenye kundi la *kutengeneza*. Watahiniwa wengine (0.4%) waliopata alama 0 walishindwa kutaja mbinu sahihi hata moja. Watahiniwa hao hawakuelewa vema matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


7. (i) Maswali na Majibu.
(ii) Onesho mbinu.
(iii) Ziara fupi.
(iv) Igizo dhima.


Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alitaja mbinu za kufundishia somo la Uraia badala ya mbinu za kupata zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia na hivyo kupata alama 0.

### 2.1.8 Swali la 8: Uchumi wa Tanzania


Mtahiniwa alitakiwa kubainisha sababu nne zinazochangia kuporomoka kwa uchumi wa Tanzania. Miongoni mwa watahiniwa 5,430 waliofanya

mtihani, watahiniwa 161 (3.0%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 503 (9.2%) walipata kuanzia alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 4,766 (87.8%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 97 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8*


Watahiniwa (87.8%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kubainisha sababu tatu hadi nne zinazochangia kuporomoka kwa uchumi wa Tanzania. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya *Uchumi wa Tanzania* hususan mada ndogo ya *Mambo yanayochangia kukua na kuporomoka kwa Uchumi*. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na watahiniwa ni kama; *rushwa, magonjwa na migogoro mbalimbali kama ya kiuchumi, kijamii na kisasa, uhaba wa mitaji, majanga ya asili* na *miundo mbinu mibovu*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8

Watahiniwa (8.4%) waliopata ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Mapungufu hayo ni kama; kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kurudia hoja na kutoa hoja pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (2.4%) waliopata ufaulu hafifu walikuwa na maarifa hafifu kuhusu *mambo yanayochangia kukua na kuporomoka kwa uchumi wa Tanzania* na hivyo kutoa hoja pungufu ya mbili au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa (0.6%) waliopata alama 0 baadhi yao hawakuwa na maarifa kabisa kuhusu dhana husika na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha sababu hizo kama; *uvuvi mbaya, kilimo cha kuhamahama* na *ukataji miti* dhana ambazo hazikuwa na nguvu kama sababu zinazochangia kuporomoka kwa uchumi wa Tanzania. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.





Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alitaja sababu za kubuni bila maelezo na hivyo alipata alama 0. Mtahiniwa hakuwa na maarifa kuhusu dhana husika na kuishia kutoa majibu ambayo alishindwa kuyatolea maelezo.

### 2.1.9 Swali la 9: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia


Mtahiniwa alitakiwa kutaja matatizo manne yanayoweza kutokea iwapo wanafunzi watakosa vitabu vya kiada vya kujifunzia somo la Uraia. Kati ya watahiniwa 5,430 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 155 (2.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 280 (5.1%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 4,995 (92%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 97.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na.** *9: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9*

Watahiniwa (92%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kutaja matatizo matatu hadi manne yanayoweza kutokea iwapo wanafunzi watakosa vitabu vya kiada vya kujifunzia somo la Uraia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Uchambuzi wa kitabu cha kiada* na walielewa vema matakwa ya swali. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa katika swali hili ni kama zifuatazo; *wanafunzi kushindwa kujijengea stadi za kujifunza, wanafunzi kushindwa kuchanganua mada inayofundishwa, wanafunzi kushindwa kujijengea maarifa mbalimbali na ufahamu kwa yale wanayojifunza* na *wanafunzi*


*kushindwa kujifunza kwa wakati wao wenyewe na kujibu maswali na kujiandalia nukuu za somo husika*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi katika swali hili.


9. Matatizo yanayoweza kutokea iwapo mwanafunzi watakosa vitabu vya kiada vya kujifunzia somo la uraia.
i) Wanafunzi watashindwa kupata mazoezi ya kutosha ili kuweza kujipima.
ii) Wanafunzi watashindwa kujifunza kwa mtiririko sahihi kwani mada hazijapangiliwa kwa usahihi kuanzia mada rahisi kwenda mada ngumu.
iii) Wanafunzi kushindwa kutathmini ujifunzaji wao.
iv/ Wanafunzi kukosa mifano ya kutosha pamoja na picha mbalimbali kuhusiana na mada.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9

Watahiniwa (5.1%) waliopata ufaulu wa wastani, wengi wao walitaja hoja pungufu na wengine kurudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha katika kundi hili wapo waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa (2.9%) waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao walitoa hoja pungufu ya mbili au walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa wengine (1.2%) waliopata alama 0 walishindwa kabisa kubaini matatizo yanayoweza kutokea iwapo wanafunzi watakosa vitabu vya kiada vya kujifunzia somo la Uraia. Watahinwa hao walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana husika na hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.




| | |
|---|---|
| 9 | i/ Somo kutoelewekua, kwani mwalimu atakosa nukuu |
| | ii/ Mwalimu kutofikia malengo, kwani atakosa mpangilio mzuri wa ufundishaji kwa kukosa nukuu nzuri za somo |
| | iii/ Mwalimu atakosa mpangilio mzuri wa ufundishaji |

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutaja mambo yanayoweza kutokea iwapo mwalimu atakosa kitabu cha kiada badala ya mwanafunzi, hivyo kupata alama 0.

### 2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya Kufundisha somo la Uraia

Swali hili lilikuwa na sehemu mbili (a) na (b). Mtahiniwa alitakiwa (a) Kutoa maana ya azimio la kazi na (b) Katika aya moja, kuonesha uhusiano uliopo kati ya muhtasari na azimio la kazi katika somo la Uraia. Miongoni mwa watahiniwa 5,430 waliofanya mtihani, watahiniwa 40 (0.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 368 (6.8%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 5,022 (92.5%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 99.3 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

Asilimia 92.5 ya watahiniwa waliofanya vizuri katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, pengine ni kwa sababu dhana hii hufundishwa katika masomo yao mengine upande wa Utaalamu. Watahiniwa hao waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa hoja sahihi tatu hadi nne. Majibu sahihi ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: kipengele (a) *Azimio la kazi ni mpango wa ufundishaji unaoandaliwa na mwalimu kutoka katika muhtasari wa somo ili kufundishia kwa muda maalum kama wiki, nusu muhula au muhula mzima*. Wakati baadhi ya hoja sahihi kwa kipengele (b) ni kama; *Muhtasari na Azimio la kazi vinahusiana kwa karibu kwani ili mwalimu aweze kuandaa azimio la kazi yampasa achambue muhtasari ili kuweza kupata malengo ya ufundishaji, mada, vitendo vya kufundishia na kujifunzia na vifaa vya kufundishia na kujifunzia*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


10. (a) Azimio la kazi
ni mpango kazi wa muda mrefu anaouandaa mwali-
mu wa somo la Uraia unaotaja kwa kifupi idadi
ya mada kwa mpangilio, zinazotakiwa kufundishwa
katika darasa husika kwa kipindi cha mwaka mzima
au muhula.

(b) Uhusiano kati ya muhtasari na azimio la kazi ni;
Ili uweze kuandaa azimio la kazi ni lazima
uwe na muhtasari wa somo husika, kwasababu
Muhtasari ndio unampa mwongozo mwalimu wa somo
la Uraia kuweza kubaini mada, malengo ya somo
na vitu vyote anavyotakiwa mwalimu katika azimio
la kazi vinavyohusiana na suala la Ufundishaji na
Ujifunzaji wa somo la Uraia.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10

Aidha, asilimia 6.8 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5, wengi wao walijibu kipengele (a) na kushindwa kujibu kipengele (b) kwa usahihi na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.7%) waliopata alama hafifu, baadhi yao walichanganya dhana ya andalio la somo na azimio la kazi au shajara ya somo, hivyo kupata alama hafifu. Wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana husika na hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.



10 a) Azimio la Kazi, ni daftari analotumia mwalimu katika kujaza taarifa za masomo ya kila siku aliyofundisha.

b) Muhtasari | ANDALIO LA KAZI

Muhtasari katika somo la uraia imehusisha maudhui, utangulizi, idadi ya vipindi na madhumuni.

Lakini Andalio la kazi la uraia imehusisha idadi ya vipindi, mahiri, shughuli za kutendwa, Umahiri, shughuli kuu na ndogo pamoja na zana za ufundishaji

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10


Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alichanganya (a) maana ya azimio la kazi na shajara ya somo na (b) badala ya kuonesha uhusiano uliopo kati ya muhtasari na azimio la kazi, alitoa tofauti kati ya muhtasari na azimio la kazi bila kuonesha uhusiano uliopo na hivyo kupata alama 0.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata kuanzia alama 6 hadi 10 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Dola

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua misingi sita ya uwepo wa demokrasia katika nchi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,757 sawa na asilimia 87.4 ya watahiniwa 5,430 waliofanya Mtihani wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa waliochagua kujibu swali hili, watahiniwa 106 (2.2%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5, watahiniwa 1,153 (24.3%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 3,501 (73.5%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 97.8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15. Chati Na.11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Watahiniwa (73.5%) waliopata alama za juu katika swali hili walikidhi matakwa ya swali kwa kufafanua misingi ya uwepo wa demokrasia katika nchi kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua misingi ya demokrasia kwa kutoa hoja kama; *uchaguzi unaozingatia Katiba ulio huru na wa haki, uwazi, uwajibikaji, utawala wa sheria, mgawanyo wa madaraka* na *kuheshimu haki za binadamu*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha katika mada husika na walielewa matakwa ya swali. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


11. Demokrasia; Ni serikali ya watu iliyo Chaguliwa na watu kwa manufaa ya watu wenyewe. demokrasia hii imegawanyika katika aina kuu mbili ambazo ni demokrasia ya watu wote na demokrasia ya uwakilishi. Nchini Tanzania tunatumia demokrasia ya uwakilishi kupitia uchaguzi wa Viongozi Mbalimbali katika Kada tofautitofauti. Ili nchi iwe na sifa ya Kidemokrasia lazima kuwepo na Misingi ambayo huashiria uwepo wa demokrasia misingi hiyo ni:-

Utawala bora; Ni hali ya kuongoza kwa kufuata kanuni na sheria zilizowekwa kwa kuzingatia katiba ya nchi; ndani ya nchi ili kuwepo na demokrasia lazima Viongozi ufuate masharti ili kutoweza kuwaumiza wananchi wake. Mfano utawala unao zingatia utu wa mtu.

Uchaguzi huru na wa haki:- Kuchagua ni kitendo cha kumpendekeza mtu atakaye simamia sheria na Kanuni zilizo wekwa ndani ya eneo husika. katika nchi zenye kufuata sera ya demokrasia lazima wananchi wawe huru katika kumchagua Kiongozi wanayempenda na kiongozi aliye chaguliwa anahaki ya kukata rufaa kama atakuwa hajaliZika.

Kuheshimu madaraka Pamoja na ugawaji wa madaraka katika Kada au vitengo Mbalimbali:- Nchi yenye hadhi ya Kidemokrasia lazima ndani yake kuwe na mgawanyo wa madaraka na pia kuheshimu madaraka ya mtu aliyopewa ili kuweza kutenda Kazi zake kwa weledi na ufasaha.

Kuzingatia Haki za binadamu; Haki ni jumla ya stahiki au mambo yote ambayo mtu anatakiwa kutendewa kutokana na hadhi ya utu wake. binadamu anatakiwa kuheshimiwa kutokana na kuwa Kiumbe Chenye utashi na kuweza kupewa stahiki zake. Mfano wa haki ambazo binadamu anatakiwa kuzipata ni Kupata Elimu, Haki ya kuoa au kuolewa, Haki ya kuchagua au kuchaguliwa.



11 Haki na Usawa:- Usawa ni hali ya kuwepo kwa utoaji au upokeaji wa huduma kwa uwiano mzuri bila ya kubaguana. Katika maendeleo ya demokrasia katika nchi lazima kuwepo na kuheshimiana bila kuwepo ubaguzi wa aina yoyote kutokana na tofauti za kidini, kikabila wala kijinsia. ndani ya nchi kukiwa na msingi wa usawa ni dhahiri kuwa basi demokrasia ipo katika nchi husika.


Kuheshimu na kufuata matakwa ya katiba ya nchi:- Katiba ni muongozo, kanuni au sheria zilizowekwa ili kuweza kufuatwa katika kuongoza nchi. katiba hii yaweza kuwa ya maandishi au ya kimapokeo. kwa kuwa katiba hutungwa na watu wenyewe ni dhahiri kuwa lazima waifuate ili kuhakikisha kuwa wanaishi katika mazingira bora na yenye usalama.

Uwepo wa demokrasia katika nchi kunahitaji msingi ambayo itaweza kufuatwa au kutekelezwa ili wananchi waweze kunufaika na sera ya demokrasia katika nchi yao. Mbali na hayo nchi zenye mfumo wa kidemokrasia huweza kunufaika katika mambo mengi ingawa huambatana na changamoto kama vile rushwa, uchuwa madaraka na ubinafsi ili kuweza kuzitatua changamoto hizo jamii inatakiwa kuelimishwa juu ya madhara haya yatokanayo na vikwazo hivyo vya demokrasia

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11

Watahiniwa (24.3%) waliopata kuanzia alama 6 hadi 10 katika swali hili, baadhi yao walidhihirisha kuwa na maarifa ya wastani katika dhana ya *Utawala wa Kidemokrasia*, hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja mbali na majibu sahihi, alichanganya majibu ambayo si sahihi kama; *kusali kwa dini yoyote* na *amani*, bila ufafafanuzi wa hoja hizo na hivyo kupata alama pungufu. Wengine walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali katika insha zao kama; utangulizi usiojitosheleza, kushindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha kutetea hoja zao, kurudia hoja yenye maana moja na hitimisho lisilo na uhusiano na swali na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa (2.2%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5, baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana iliyoulizwa, hivyo kutoa majibu pungufu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo kupata alama hafifu. Aidha, watahiniwa wawili (2) waliopata alama 0 mmoja hakuwa na maarifa kabisa kuhusu dhana ya *Utawala wa Kidemokrasia* na hivyo kutoa majibu ya kubuni yalisababisha kushindwa kwake. Mtahiniwa huyu alitoa hoja kama; *siasa za ndani, amani na utulivu* na *uhuru na mshikamano.* Aidha mtahiniwa mwingine hakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu yasiyoendana na swali. Kielelezo Na. 11.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali hili.



11. Demokrasia ni jumuiya ya watu iliyoundwa na watu kwa ajili ya watu. Huundwa na bunge na kukubaliwa kutumika kwa ajili ya wananchi.

Ifuatayo ni misingi ya uwepo wa demokrasia katika Nchi.

Kupitisha bajeti: Bunge linapanga bajeti ya Nchi kwa siku ishirini na tisa, kwa mwaka mara moja. hii ni kutokana na upangiliaji wa bajeti kwa ajili ya mambo mbalimbali katika Nchi mfano ujenzi wa shule na zahanati za kijiji, hospitali kubwa za mkoa na ukarabati wa vituo vya kulelea watoto yatima na kusaidia mama wajawazito.

Kumtoa raisi madarakani: Hii hutokea baada ya raisi kukiuka baadhi ya sheria kama vile kukataa mswada uliopitishwa na bunge. Anaemtoa raisi madarakani ni bunge na sio vinginevyo.

Kupitisha mswada: Hii hupitishwa na bunge kwani kutokana na raisi kuapishwa, mswada nao unapitishwa ili kuashiria kuwa watu wote wamemkubali raisi.

Demokrasia ya Nchi ni muhimu kwani husaidia wananchi katika mambo mengi bungeni. Hivyo basi uwepo wa demokrasia katika nchi husaidia katika kupitisha bajeti, mswada na kumtoa raisi madarakani.


Husaidia katika soko huria: Soko huria ni soko huru ambapo kila mtu yuko huru kuuza chochote kwa bei elekezi.

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11

Katika Kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa alifafanua baadhi ya kazi za Bunge badala ya misingi ya uwepo wa demokrasia katika nchi.

### 2.2.2 Swali la 12: Utamaduni Wetu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kupendekeza njia tano za kukabiliana na athari ya ukuaji wa sayansi na teknolojia kwenye mila na desturi za Watanzania. Kati ya watahiniwa 2,229 waliochagua kufanya swali hili, watahiniwa 107 (4.8%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5. Watahiniwa 1,045 (46.9%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 1,077 (48.3%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 95.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa* katika swali la 12

Watahiniwa (48.3%) waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5 walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya *Utamaduni wa Kigeni*. Watahiniwa hawa walielewa matakwa ya swali na pia walitoa hoja sahihi kulingana na matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa katika swali hili ni kama; *kuacha kuiga mila na desturi za kigeni zisizofaa kwa mfano, uvaaji wa mavazi yasioendana na mila na desturi za Kitanzania, kutoa elimu juu ya mila na desturi za watanzania, kutoa malezi bora, kutunga sheria* na *kushirikisha jamii yote pamoja na vyombo vya dola*. Kielelezo

Na. 12.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

12. Mila ni mambo mbalimbali yanayofanyika katika jamii fulani na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Na desturi ni mambo mbalimbali yanayo fanyika kwa muda mfupi na kupotea katika jamii mbalimbali. Mfano uvaaji wa mavazi mbalimbali, matumizi ya vyakula mbalimbali na kadhalika.

Zifuatazo ni njia mbalimbali za kukabiliana na athari ya ukuaji wa Sayansi na Teknolojia kwenye mila na desturi za Watanzania;

Kutoa elimu kwa jamii juu ya athari mbalimbali za ukuaji wa Sayansi na teknolojia kama vile kutoa elimu juu ya mavazi ya kujisitiri hasa kwa vijana.

Kuweka vikomo juu ya matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii; Wizara ya mawasiliano ~~it~~ inatakiwa kuweka kikomo katika matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ili kudhibiti maadili

Kuepuka desturi potofu zinazoathiri mila na desturi za watanzania; Watanzania wanatakiwa waepuke kuiga mambo mbalimbali ambayo hayajengi, Mfano, katika mavazi, vijana wengi siku hizi wanavaa kama wazungu hivyo hudhorotesha mila na desturi za Watanzania


Kuanzishwa kwa masomo ya maadili ya Kitanzania katika shule za msingi hadi sekondari ili kuweza kuwajenga wanafunzi katika misingi na makuzi yanayokubalika katika jamii.

Wazazi washauriwe jinsi ya kuwadhibiti watoto wao katika matumizi mbalimbali wa vifaa vya mawasiliano kama, runinga, tarakilishi na simu, wazazi wengi siku hizi huwanunulia watoto wao simu wakiwa bado wadogo hivyo kwa namna yoyote mtoto hataweza kuacha kuvitumia.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12

Watahiniwa (46.9%) waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walishindwa kutoa maelezo sahihi katika kutetea baadhi ya hoja zao na wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye kujitosheleza. Miongoni mwao, wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na hivyo kupata alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja ambazo si sahihi kwenye majibu yake kama; *kuwapa watoto mifano*, *kuwasisitiza watoto wasome kwanza*, bila ya maelezo yenye kuziunganisha na kiini cha swali, hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa (4.8%) waliopata alama hafifu katika swali hili, kati yao wapo waliokuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo kutoa hoja dhaifu bila maelezo ya kina na wengine kati yao walitaja hoja bila kutoa ufafanuzi, utangulizi wala hitimsisho. Wengine walibainika kukosa maarifa kabisa kuhusiana na dhana husika na hivyo kutoa majibu yasiyosahihi yaliyosababisha kushindwa kwao. Hata hivyo, watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu tofauti na dhana iliyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maeneo ya mila na desturi za Watanzania yaliyoathirika na ukuaji wa sayansi na teknolojia badala ya mbinu za kukabiliana na athari hiyo kwa hoja kama; *mavazi*, *chakula*, *lugha* na *sherehe*. Kielelezo Na. 12.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


12. Mila na desturi Hizi ni Mila ambazo ziko katika kila jamii nchi Tanzania hazijaweza kubadilika tangu hapo kale. Mambo yanayoathiri ukuaji wa ukuaji na Sayansi na teknolojia kwenye Mila na desturi ni.

Mmomonyoko wa Maadili Katika jamii Maadili yamekuwa ni athari kubwa ya kufahamika nalo kwa sababu dunia imekuwa kama kijiji kwa sababu ya Sayansi na teknolojia kuongezeka katika Mila na desturi za watanzania vijana kufanya yasiyofaa katika mitindo mbalimbali.

Kuongezeka kwa vitendo vya wizi katika ukuaji wa Sayansi na teknolojia vitendo vya wizi vimeathiri sana katika jamii kwa sababu ni ukuaji wa mila na desturi za kitanzania inabidi kukubaliane na janga hili kuwepo na vitendo vya uharifu.

Ukeketaji wanawake katika baadhi ya jamii za kiafrika mila na desturi zimeathiriwa sana kuamini mwanamke ili aweze anapoolewa katika ndoa yake lazima afanyiwe ukeketaji kwa hiyo Sayansi imekuwa imeathiri jamii kwa hiyo kilelimu kielimu inabidi tukubaliane na desturi za watanzania.

Kurithi wajane katika ukuaji wa Sayansi na teknolojia za mila na desturi za watanzania jamii nyingi zinaamini kuwa kila mwanamke wa kaka yako au ndugu yako alafa lazima umurithi hizo ndio mila haziwezi kubadilika katika nchi ya Tanzania.


Ongezeko la watoto mitaani hii pia ni moja ya athari ya kukabiliana nayo katika mila zetu za desturi za watanzania kwa sababu katika nchi yetu au jamii yetu kuna watoto wengi ambao wengi wazazi watoto hawajui baba yao au mama yao ni nani au yuko wapi hili kukabiliana na Sayansi ya teknolojia

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12

Katika Kielelezo Na.12.2 mtahiniwa alichanganya baadhi ya mila zisizofaa kama; *ukeketaji wa wanawake*, *urithi wajane* na athari mbalimbali za kuiga mila za kigeni badala ya kupendekeza njia za kukabiliana na athari ya ukuaji wa sayansi na teknolojia kwenye mila na desturi za Watanzania na hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.3 Swali la 13: Uhusiano wa Kimataifa

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua mchango wa Umoja wa Mataifa katika ustawi wa nchi wanachama kwa kutoa hoja tano. Kati ya watahiniwa 3,860 waliochagua kufanya swali hili, watahiniwa 64 (1.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5. Watahiniwa 371 (9.6%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 3,425 (88.7%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.3 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa* katika swali la 13

Watahiniwa (88.7%) waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 15 walielewa vema matakwa ya swali na hivyo waliweza kuchambua mchango wa Umoja wa Mataifa katika ustawi wa nchi wanachama. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kina kuhusu mada ndogo ya *Maeneo ya Mahusiano ya*

*Kimataifa*. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili ni kama ifuatavyo: *Hutoa sera na miongozo ya kusimamia nyanja mbalimbali za kimataifa katika uendeshaji wake, kuandaa programu za maendeleo za kimataifa ambazo hutoa miongozo kwa nchi wanachama ili kufikia maendeleo hayo, kusaidia katika kutatua majanga yanayokumba nchi wanachama kupitia mashirika yake* na *kuandaa programu za ulinzi na usalama kwa jamii ya kimataifa.* Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


13 Umoja wa Mataifa (UNO) Ni jumuiya ambayo ilianzishwa mwaka 1945 baada ya Vita ya Pili ya dunia kwa lengo la kuzuia kutokea kwa vita ya tatu ya dunia. Mchango wa umoja wa mataifa ;- Ni jitihada za maksudi zinazofanywa na jumuiya hii ili kuweza kuleta maendeleo kwa nchi wanachama. Ifuatayo ni michango ya umoja wa Mataifa katika ustawishaji wa nchi wanachama michango hiyo ni ;-

Kutatua migogoro mbalimbali kati ya nchi wanachama ;- umoja wa mataifa kwa kiasi kikubwa unasaidia katika kushughulikia migogoro kati ya nchi wanachama ikiwemo migogoro ya kimipaka, kivita ili kuweza kusaidia kuondoa tofauti baina ya nchi wanachama.

Kuanzisha mashirika mbalimbali ya kutoa huduma kwa nchi wanachama; Mfano Benki ya dunia, shirika la wakimbizi UNHCR, shirika la wafanya kazi ILO na shirika la Chakula duniani FAO, yote haya yalianzishwa chini ya umoja wa Mataifa kwa lengo la kutoa huduma Mbalimbali kwa nchi wanachama ili waweze kunufaika.

Kutoa misaada Mbalimbali kwa nchi wanachama walioathiriwa na majanga: Mfano kutoa Chakula, fedha, na Madawa. Umoja wa mataifa unamchango mkubwa kwa nchi wanachama walioathiriwa na Majanga mbalimbali ili kuweza kuepuka kuporomoka kwa uchumi wa nchi husika.

Kusimamia ulinzi na usalama kwa nchi wanachama; Mfano uwepo wa wanajeshi wa umoja wa mataifa wanao hakikisha ulinzi katika mataifa yenye vuguvugu za kivita. Mfano nchini Kongo, na Sudani ; Kupitia kuwepo kwa umoja wa mataifa askari wake wameweza au wanasaidia katika kukomesha vurugu na kukamata magenge yote ya uharifu katika nchi wanachama ili kuleta amani.


13. Kuhamasisha maendeleo katika nchi wanachama: Umoja wa mataifa kama shirika linasaidia katika kuhamasisha maendeleo endelevu katika nchi wanachama ikiwemo ujenzi wa viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa pia ujenzi wa Miundombinu ambayo itasaidia kuhimalisha uchumi wa nchi.

Kutetea na kusimamia haki za binadamu; kupitia umoja wa kimataifa haki mbalimbali za raia huweza kufuatwa na kusimamiwa ili kuweza kuwa na usawa kutokana na matakwa ya nchi husika.

Umoja wa mataifa unamchango mkubwa sana kwa nchi wanachama ili kuweza kuhamasisha maendeleo endelevu katika nchi mbalimbali, ingawaje shirika hili huweza kukumbwa na changamoto kama vile rushwa, ubadhilifu wa mali za umma.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13

Watahiniwa (9.6%) waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, baadhi yao waliweza kutoa utangulizi sahihi lakini walishindwa kuchambua vizuri hoja zao na wengine walitoa hoja pungufu hivyo kupata ufaulu wa wastani.

Asilimia 1.7 ya watahiniwa waliopata alama za chini katika swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kina kuhusu dhana iliyoulizwa na hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyosahihi. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kuandika majibu yasiyohusiana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika tabia za utandawazi kwa hoja kama; *kuondoa vikwazo vya kibiashara*, *unahimiza soko huria*, *unasisitiza utunzaji wa mazingira* na *unasisitiza usawa wa kijinsia*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zisizokuwa na mahusiano na kiini cha swali kwa hoja kama; *kusimamia utekelezaji wa majukumu na Katiba*, *kudumisha amani na upendo katika nyanja za uchumi, afya na maendeleo* na *kutatua mgogoro wa jamii*. Mtahiniwa huyu pia alishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye kujitosheleza na hivyo alipata alama 0.

Kielelezo Na. 13.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya maarifa na hivyo kushindwa swali hili.

13. Umoja wa Afrika ni muungano wa nchi huru za kiafrika kwa malengo mbali mbali mfano maendeleo ya kiuchumi
Ifuatayo ni michango ya umoja wa Afrika katika ustawi wa nchi wana chama
Kusaidia nchi wanachama katika kukuza uchumi wa nchi. mfano: Tanzania na Rwanda.
Kusaidia katika kukabiliana na migogoro na umaskini miongoni mwa nchi wanachama mfano migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii
Kusaidia katika kubadilisha ujuzi maarifa na stadi katika mambo ya tekno lojia ya sasa mfano stadi za kuunda na kutengeneza vitu mbalimbali
Vilele kushirikiana katika kupambana na magonjwa sugu mfano UKIMWI, Ebora na Korona yanayotikisa ulimwengu wa sasa.

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 13


Katika Kielelezo Na. 13.2 mtahiniwa aliandika mchango wa jumuiya ya Afrika kwa nchi wanachama badala ya mchango wa Umoja wa Mataifa katika ustawi wa nchi wanachama.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu)

Katika sehemu hii kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata kuanzia alama 6 hadi 10 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

### 2.3.1 Swali la 14: Uchambuzi wa Mchapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia


Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza vigezo sita vya kuzingatia katika kubaini machapisho bora ya ziada katika somo la Uraia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2,056 (37.9%) kati ya watahiniwa 5,430 waliofanya mtihani wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa waliofanya swali hili, watahiniwa 168 (11.8%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,182 (55.3%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 677 (32.9%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 88.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14*

Watahiniwa wengi (55.3%) waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walitoa hoja pungufu pamoja na baadhi ya maelezo yasiyokuwa na mahusiano na swali. Wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kwa mfano, mtahiniwa mmoja mbali na hoja sahihi alizotoa pia alitoa hoja kama; *yaonyeshe zana*, *yawe na maswali ya upimaji mwisho* na *kuzingatia ubora wa machapisho;* hoja ambazo hazikuwa sahihi na hivyo kupata alama pungufu. Aidha, wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza.

Watahiniwa (32.9%) waliopata alama nzuri katika swali hili, waliweza kueleza vigezo vitano hadi sita vya kuzingatia katika kubaini machapisho bora ya ziada katika somo la Uraia. Watahiniwa hao pia walidhihirisha kuwa na uwezo mzuri katika uandishi wa insha kuanzia kwenye utangulizi hadi hitimisho. Baadhi ya majibu ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa kama; *yawe na uhusiano na mada za somo la Uraia, lugha inatakiwa kuwa sahihi na rahisi kwa wanafunzi kuelewa, yazingatie utamaduni sahihi wa wanafunzi, yasiwe yenye lugha ya upendeleo, upotoshaji na matusi* na *yawe yanapatikana*. Kielelezo Na. 14.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



14 Machapisho bora ya ziada ni vitabu, majarida, magazeti na matini mbali mbali yanayotumiwa na mwalimu na mwanafunzi kwa lengo la kumuongezea maarifa ya ziada au kujibidiisha. Zifuatazo ni vigezo muhimu vya kuzingatia katika kubaini machapisho bora ya ziada katika somo la uraia.

Lugha iliyotumika inatakiwa kuwe fasaha au sahihi. Machapisho ya ziada yanatakiwa kuwa na lugha ambayo inaweza kutumiwa na mwanafunzi na mwalimu katika kuyatumia.

Yawe na maudhui ya somo la uraia kutoka kwenye muhtasari wa somo la uraia. Malengo makuu ya mada husika yanatakiwa kuwepo na kuchambuliwa kwa kina zaidi hili yaweze kumuongezea maarifa wanafunzi.

Yawe na vielelezo vya picha na michoro inayoangalia usawa wa kijinsia. Hisiwe na picha au michoro inayoonesha jinsi moja mabaya tu bali inatakiwa kuangalia mambo ya kijinsia katika michoro na picha.

Yawe na maadili yanayoendana na jamii husika au nchi zima. Hiweze kuangalia utamaduni wa jamii inayotumika. Wanafunzi au mwalimu anaetumia.

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (11.8%) walipata alama 0 hadi 5.5. Baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo waliweza kuandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzitetea, hivyo kupata alama za chini. Wengine (0.2%) waliopata alama 0, kati yao wapo ambao hawakuwa na maarifa kabisa kuhusiana na dhana husika na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *umri wa watoto na uelewa wa watoto*, *idadi ya wanafunzi*, *ukubwa wa darasa* na *muda wa kutumia* ambayo ni mambo ya kuzingatia katika kuchagua mbinu ya kufundishia au kutengeneza zana. Kielelezo Na.14.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


14. Zifuatazo ni Vigezo anavyotakiwa kuzingatia mwalimu anapotaka kubaini machapisho ya ziada
Kuhudhuria Semina na makongamano, ili mwalimu aweze kupata machapisho ya ziada anapaswa kuhudhuria Semina mbalimbali na mikutano mayohusiana na masuala ya kiserikali, kuchumi na kijamii na kunukuu hoja na mawazo ya watu tofauti tofauti.
Kudhuru maktaba, ili mwalimu aweze kupata machapisho ya zaida anapaswa kudhuru katika maktaba mbalimbali ili kuweza kupata nukuu kutoka kwenye vitabu na tafiti za watafiti mbalimbali.
Kufanya tafiti mbalimbali kuhusiana na Somo la Uraia, mwalimu anapaswa kuwa mdadisi kwa kutafiti mambo mbalimbali yanayohusiana na ukweli kuhusu Somo la Uraia ili kuweza kupata ukweli wa mambo hayo.
Kufuatilia vyombo vya habari, mwalimu pia anaweza kupata machapisho ya ziada kwa kusikiliza redio, kuangalia runinga ~~na~~ ~~ka~~ anaweza kupata na kujua ukweli kuhusu masuala yanayohusiana na Somo la Uraia
Kutumia/kutafuta ukweli kutoka kwenye mitandao ya kijamii mfano "youtube" "twitter" na "google" anaweza kupata machapis

Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.2 mtahiniwa alieleza njia za kutafuta machapisho bora ya kujifunzia somo la Uraia badala ya kueleza vigezo vya kuzingatia katika kubaini machapisho bora ya ziada katika somo la Uraia.

### 2.3.2 Swali la 15: Zana za kufundishia na Kujifunzia

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua matumizi sita ya zana za kufundishia na kujifunzia. Kati ya watahiniwa 5,219 waliochagua kufanya swali hili, watahiniwa 37 (0.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa 276 (5.3%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 4,906 (94%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 99.3 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 15.




**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15*

Watahiniwa wengi (94%) waliopata alama za juu katika swali hili, waliweza kufafanua matumizi matano hadi sita ya zana za kufundishia na kujifunzia kulingana na matakwa ya swali. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia*. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *hutumika kumsaidia mwalimu kuwaelewesha wanafunzi wake dhana ngumu na yenye utata*, *hutumika kumsaidia mwalimu kujenga kumbukumbu kwa wanafunzi wake*, *huokoa*

*muda katika ufundishaji wa dhana husika* na *hutumika katika kupunguza maelezo marefu toka kwa mwalimu*. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

15. Zana za kufundishia na kujifunzia ni vifaa anavyovitumia mwalimu ili kuraisisha ufundishaji wake katika uwasilishaji wa maudhui ya somo husika. Yafuatayo ni matumizi ya Zana za kufundishia na kujifunzia :-


Hutumika kuraisisha ufundishaji na ujifunzaji; Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji mwalimu anapotumia kutumia zana ili kumfanya mwanafunzi kuelewa kwa urahisi kwani anapoona kitu kinachozungumziwa ataweza kutunza kumbukumbu ya matumizi ya kitu hicho ili hata akikiona sehemu aweze kukitumia.

Hutumika kuchochea udadisi kwa mwanafunzi; kupitia Zana za kufundishia na kujifunzia kutamfanya mwanafunzi awe mdadisi juu ya zana inayotumika kwa kuhoji matumizi ya zana hiyo, inahusianaje na maudhui ya kujifunza. hii pia itamfanya atumie kumbukumbu na aelewe kwa undani zaidi kupitia zana iliyotumika.

Hutumika kuvuta usikivu kwa mwanafunzi; Kutokana za kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji mwalimu ataweza kuvuta usikivu kwa wanafunzi kwani atakapokuwa ameibandika au ameningʼinizia zana ubaoni wanafunzi watakapoona watatulia na kutafakari kuhusiana na zana hiyo.

Kukuza ari ya wanafunzi kupenda kujifunza; katika ujifunzaji wanafunzi hupenda sana kushirikishwa, hivyo mwalimu anapofundisha kwa kutumia zana na anawashirikisha wanafunzi katika kutenda, hii itawafanya wapende kujifunza zaidi kupitia zana tofauti tofauti anazotumia mwalimu kwani baadhi ya zana huwa zina mvuto kwa wanafunzi.

Hutumika kujenga kumbukumbu kwa mwanafunzi; Mwanafunzi anapokuwa anajifunza kwa kutumia zana ataweza kutunza kumbukumbu kwani kupitia zana hizo anakuwa anatenda pia hata asipotenda anakuwa anaona kwa mwalimu anapokuwa anatolea zana husika maelezo au jinsi inavyotumika.


15 Hutumika kuokoa muda katika ufundishaji; Matumizi
ya zana katika ufundishaji na ujifunzaji yanaokoa muda kwani
wanafunzi wanakuwa wanaelewa kwa urahisi wanapokuwa wanahusianisha
zana na maneno au maelezo anayotoa mwalimu. Tofauti na kama
mwalimu angeelezea tu bila kutumia zana angetumia muda-
mwingi.
Zana za kufundishia na kujifunzia zina hasara zifuat-
azo wakati wa kuziandaa kwanza zinatumia gharama, zana
zingine zinatumia muda mwingi kuziandaa.

Kielelezo Na. 15.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 15

Aidha, watahiniwa (5.3%) waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walishindwa kufafanua matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia kwa usahihi na wengine walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kutetea hoja zao. Aidha wapo walioshindwa kutoa maelezo sahihi ya utangulizi na hitimisho na wengine walitoa hoja pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.7%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu *matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia* na hivyo kushindwa kutoa hoja zilizohitajika.Wengine (0.1%) waliopata alama 0, hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika na kati yao hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *hutumika katika tafiti za kielimu*, *hutumika kuandaa mwongozo wa upimaji* na *hutumika kuandaa azimio la kazi na nukuu za somo*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama; *utangulizi vema, hutumika kujengea maarifa mapya, kuimarisha maarifa, kuhitimisha na kufanya tathmini;* ambayo yote si majibu sahihi. Kielelezo Na. 15.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

15 Zana; Ni vifaa vya kisasa au visivyo vya kisasa viandaliwavyo au vinavyoandaliwa na mwalimu pamoja na mwanafunzi ili vitumike katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa.

Zifuatazo ni sifa za zana ~~bora~~ za kufundishia na kujifunzia;

Iendane na shughuli ndogo au lengo mahususi linalokwenda kufundishwa; Hii ni sifa mojawapo ya zana bora kwa sababu isipoendana na kile kinachofundishwa lengo mahususi halitofikiwa.

Iwe inayovutia; Zana bora ni ile inayovutia na isio inayotisha ili mtoto au mwanafunzi ajifunze bila woga au wasiwasi mwalimu anapaswa kuandaa zana itakayo wavutia wanafunzi

Iendane na Umri na Uelewa wa mlengwa; katika ulazi au maandalizi ya zana mwalimu anapaswa kuzingatia umri na uelewa wa wanafunzi wake wakati ili asije andaa zana iliyojuu ya uwezo wao.

Isiwe hatarishi; Mwalimu anapaswa kuzingatia usalama wa watoto au wanafunzi katika maandalizi ya zana za kufundishia na kujifunzia

Imshirikishe mtoto katika tendo la ujifunzaji; Mfano kama ni kugusa mtoto anapaswa aiguse, aibebe, aichunguze ili kumjengea kumbukumbu na stadi ya ubunifu.


Iwe kubwa na imara kulingana na idadi ya watoto darasani; Zana inapaswa kuonekana kwa wanafunzi wote darasani na ikiwezekana kuhamishika kwa urahisi bila kupata hitilafu au dosari yoyote ile kutokana na uimara wa zana hiyo.

Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 15

Katika Kielelezo Na. 15.2 mtahiniwa alifafanua sifa za zana za kufundishia kwa hoja kama; *iendane na lengo mahsusi* na *iwe inayovutia* badala ya kufafanua matumizi ya zana za kufundishia.


### 2.3.3 Swali la 16: Upimaji na Tathmini

Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia hoja sita, kuonesha matumizi ya alama za mtihani katika somo la Uraia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,571 (65.8%) kati ya watahiniwa 5,430 waliofanya mtihani wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa waliofanya swali hili, watahiniwa 45 (1.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 239 (6.7%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 3,287 (92%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.7 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 16.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16*

Watahiniwa wengi (92%) waliopata alama za juu katika swali hili, waliweza kubaini matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Upimaji na Tathmini* na hivyo kutoa majibu sahihi kama; *katika kuinua maendeleo ya mwanafunzi mwalimu anatumia mitihani mbalimbali kupima uwezo wa kila mwanafunzi akilinganishwa na wenzake darasani*, *huwapa wanafunzi changamoto ya kujifunza zaidi* na *hutumiwa na wadau wa elimu jinsi ya kufanya marekebisho juu ya mtaala wa somo la Uraia*. Kielelezo Na. 16.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.



16. Alama za mitihani ni alama ambazo hutolewa na mwalimu kwa wanafunzi wake baada ya kufanya mitihani na huweza kuandikwa kwa namba kwa lengo la kuonyesha ufaulu. Alama za mitihani katika somo la uraia zina matumizi mbali mbali kama vile.

Humsaidia mwalimu kufanya tathimini. Alama za mtihani wa uraia zina weza kumfanya mwalimu kujua ni kwa kiasi gani wanafunzi wake wameelewa yale aliyofundisha na kufanya tathimini ya jumla.

Humsaidia mwalimu kupanga matokeo ya wanafunzi wake darasani, Mwalimu anaweza kutumia alama za mitihani kupanga ufauru wa wanafunzi wake kuanzia wa kwanza mwenye alama za juu zaidi mpaka wa mwisho mwenye alama za chini.

Humsaidia mwalimu kuchunguza ufundishaji wake kwa kubadili mbinu anazo tumia darasani kufundisha. Kwa mfano ikiwa wanafunzi wana alama za chini sana atafanya utafiti ikiwa tatizo hawaelewi somo atatumia njia nyingine ili waweze kuelewa.

Humsaidia mwalimu kujua uwezo wa wanafunzi darasani. Alama za somo za uraia zinaweza kutumiwa na mwalimu kujua uwezo wa mwanafunzi mmojammoja katika darasa lake kisha kujua jinsi ya kuwasaidia walio chini.

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 16

Aidha, asilimia 6.7 ya watahiniwa walipata alama za wastani kwa sababu baadhi yao walishindwa kufafanua hoja kwa usahihi na walitoa hoja pungufu. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *husaidia katika kumvutia mwanafunzi*

*na somo*, *humuhamasisha mwalimu kufundisha somo la Uraia* ambazo hazikuwa sahihi kulingana na matakwa ya swali. Hata hivyo, wapo kati yao mbali na dosari mbalimbali walibainika kushindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho na hivyo kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (1.3%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana ya *Upimaji na Tathmni* na hivyo walishindwa kutoa hoja zilizohitajika. Wengine (0.6%) waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika na wengine kati yao hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu ambayo si sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika faida za alama zinazotumika kuonesha vitu mbalimbali katika jamii kwa hoja kama; *dira*, *kuonya raia*, *kutangaza* na *kuburudisha*. Mtahiniwa mwingine aliandika matumizi ya maelekezo ya mtihani kwa hoja kama; *kuonesha mahitaji ya swali*, *kuonesha vitu ambavyo havihitajiki wakati wa mtihani*, *kuonesha sehemu za mtihani* na *kuonesha maswali ambayo yanapaswa kujibiwa na maswali ambayo hayajibiwi*, badala ya matumizi ya alama za mtihani katika somo la Uraia. Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

16. Alama za mtiani, ni mbinu za ishara zitumikazo Katika uandishi na uchapishaji wa mtihani, Kunaaina nyingi za ~~aina~~ alama ambazo mara nyingi hutumiwa Katika uandishi wa mtihani. Ifuatayo ni matumizi ya alama zitumikazo Katika uandishi au uchapaji wa mitihani Katika Somo la Uraia.
Kuonesha mKazo wa neno, Kuna alama ambayo ikitumiwa Kwenye mtihani inatoa tafsiri ~~ya~~ ya msisitizo au mKazo wa neno hivyo mtahiniwa atalitilia maanani mfano wa alama hiyo " " ni alama ya fungua na funga semi alama hii hutilia mKazo wa neno
Kuonesha hali ya Kuuliza jambo, Unapokuwa unasoma neno au sentensi fulani unatakiwa uzingatie taratibu-na Kanuni za uandishi Kwa mfano utakuta sentensi-yenye alama ya Kuuliza ? alama hii hutumiKa Kuashiria Kwamba Kuna Kitu ambacho Kimeulizwa.
Kuonesha hali ya mshangao, mtu anapokuwa ametaamaKi Kuna baadhi ya alama ambazo hutumiKa ili-Kuonyesha Kweli huhusiKa ametaamaKi mfano alama hii ! alama hii huonesha ya Kuwa unachoKisoma Kipo Katika hali ya mshangao.
Kuonesha mwisho wa sentensi, alama inayotumiKa Kuonesha mwisho ni alama ya nukta • alama hii utaKutana nayo mara baada ya sentensi fulani Kufikia mwisho au KiKomo.

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 16

Katika Kielelezo Na. 16.2 mtahiniwa alieleza faida za alama za uandishi kwa hoja kama; *nukta, alama ya kuuliza* na *koma* badala ya kutoa hoja zinazoelezea matumizi ya alama za mtihani katika somo la Uraia na hivyo kupata alama 0.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa Uraia ulikuwa na maswali 16 yaliyotungwa toka mada 9 katika Muhtasari wa somo hilo, ambapo mada nne zilitoka upande wa Taaluma na mada tano upande wa Utaalamu/Ufundishaji. Ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2020 ulikuwa mzuri kwa sababu watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu katika mada zote tisa kama ifuatavyo: Mada ya *Maandalizi ya Kufundisha somo la Uraia* iliongoza kwa kuwa na ufaulu wa asilimia 99.3, ikifuatiwa na *Upimaji na Tathmini* (98.6%), Dola (98.4%), *Uhusiano wa Kimataifa* (98.3%), *Utamaduni wetu* (97.1), *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* (97.1%), *Uchumi wa Tanzania* (97.0%), *Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia* (92.7%) na mada ya *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Uraia* iliyokuwa na ufaulu wa asilimia 80.6. (Tazama kiambatisho)

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa wengi walifanya vizuri katika mada nyingi kutokana na kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Hata hivyo, walikuwepo watahiniwa wachache walioshindwa kupata alama za juu hasa katika mada za *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Uraia* na *Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia*. Baadhi ya sababu zilizopelekea kushindwa kwao ni kama ifuatavyo: Uelewa mdogo wa dhana zilizoulizwa hususan dhana nzima ya *Uhusishi wa dhana tata na uzoefu wa wanafunzi* na dhana ya *Uchambuzi wa machapisho ya ziada*. Sababu nyingine ni maarifa hafifu ya utambuzi wa matakwa ya swali na uwezo mdogo wa kufafanua hoja kwa kutumia mifano hasa katika maswali ya insha.

## 4.0 HITIMISHO

Ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa 612 Uraia 2020 ni mzuri kwa kuwa, asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya Mtihani walipata asilimia 40 na zaidi. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa katika maswali, uwezo mkubwa wa kubaini matakwa ya maswali na maarifa ya kutosha juu ya uandishi sahihi wa insha. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa zipo changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kupata alama za juu kama; uwezo mdogo wa kufafanua hoja hasa katika maswali ya insha, uelewa mdogo wa kubaini matakwa ya swali na maarifa hafifu ya dhana mbalimbali zilizoulizwa.

Taarifa hii itasaidia kuinua zaidi ufaulu katika somo la Uraia kwani itatoa msingi kwa wakufunzi na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada zilizoonekana kuwa na changamoto. Aidha, taarifa hii itatoa chachu kwa wanachuo na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za taaluma na utaalamu zilizopo katika muhtasari wa somo la Uraia.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa iwe msingi katika kuwasaidia wakufunzi na wanachuo kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali na kisha kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa wakufunzi katika ufundishaji na upimaji, na pia itasaidia kuinua zaidi ufaulu katika somo hili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi ufaulu wa watahiniwa katika somo hili inapendekezwa kuwa:

(a) Wakufunzi waandae majaribio na mazoezi ya kutosha hususan kwenye dhana ambazo hazikufanya vizuri zaidi za *Uhusishi wa dhana tata na uzoefu wa mwanafunzi* na *Uchambuzi wa machapisho ya ziada*.

(b) Walimu tarajali waongozwe katika majadiliano katika vikundi na mawasilisho na kusoma matini kuhusu dhana mbalimbali hususan za *Uhusishi wa dhana tata na uzoefu wa mwanafunzi* na *Uchambuzi wa machapisho ya ziada*.

(c) Walimu tarajali watakiwe kuchambua dhana mbalimbali za somo la Uraia na kutakiwa kuwasilisha insha ya mtu mmoja mmoja ili kuwajengea uwezo katika uandishi sahihi wa insha.

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA URAIA

| Na. | Mada | Na. ya swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Maandalizi ya kufundisha somo la Uraia | 10 | 99.26 | 99.3 | Vizuri |
| 2. | Upimaji na Tathmini | 2 | 98.43 | 98.6 | Vizuri |
| | | 16 | 98.71 | | |
| 3. | Dola | 1 | 98.07 | 98.4 | Vizuri |
| | | 5 | 99.50 | | |
| | | 11 | 97.77 | | |
| 4. | Uhusiano wa Kimataifa | 13 | 98.34 | 98.3 | Vizuri |
| 5. | Utamadunini Wetu | 3 | 99.06 | 97.1 | Vizuri |
| | | 12 | 95.20 | | |
| 6. | Zana za kufundishia na kujifunzia | 7 | 94.92 | 97.1 | Vizuri |
| | | 15 | 99.29 | | |
| 7. | Uchumi wa Tanzania | 8 | 97.03 | 97.0 | Vizuri |
| 8. | Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Uraia | 9 | 97.15 | 92.7 | Vizuri |
| | | 14 | 88.23 | | |
| 9. | Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia | 4 | 73.90 | 80.6 | Vizuri |
| | | 6 | 87.20 | | |